TUMBILI NA NYANI

JOKA naapa Jalali,
Hawi rafiki mkweli,
Nyani ni mla batili,
Kumshitaki tumbili,
nyani mnyama ayari,
kwa nisai na rijali,
haramu kwake halali,
nyani haamuwi haki.

Nyani haamui kweli,
Ni haini msaliti,
Ni muongo kukithili,
Kumshitaki tumbili,
anapokosa tumbili,
maisha hasemi kweli,
hata akiwa liwali,
nyani haamuwi haki

Mimi nilipoliwa mali,
Nikamwendea liwali,
Nikampa yule tumbili,
Kumshitaki tumbili,
mwizi wangu ni tumbili,
na mashitaka kamili,
mali kanila batili,
nyani haamuwi haki

Nyani alitahayari,
Akampa Joka vijali,
Yuko sitayasitili,
Kumshitaki tumbili,
kama msikwa kisuli,
tumbili haibi mali,
ingawa yote ni kweli,
nyani haamuwi haki

Kwaherini washairi,
Haiwezi kustiri,
Ambaye kafia mbali,
Kumshitaki tumbili,
ni mimi sanda ya mbali,
maiti aliye mbali,
mithali haikubali,
nyani haamuwi haki.

DAKO KASONGO,
MOMBASA.

ZAWADI: Meya wa Mombasa, Diwani Ahmed Shahame Mwidani anamkabidhi Bw. Caxton mwajala wa British American Insurance Co. (Kenya) Ltd. zawadi ya saa yenye thamani ya 9,000/- huku Meneja wa Kampuni hiyo, Bw. Mohammed S. Gharib akiagalia.

SHAHADA: Waziri Mdogo wa Utamaduni na Huduma za Jamii, Bw. Noah Katana Ngala (kushoto) anamkabidhi Bw. Paul Ndeda shahada ya kazi bora aliyoifanya kama Meneja wa timu ya Harambee Stars. Bw. Mahallon Danga (wapili, kulia) anaangalia.

PICHA: KENYA NEWS AGENCY

'Wimbi La Matatizo Laikumba Baraza', Adai Mahrus

BARAZA la Lamu lilijaribu liwezavyo kuwafahamisha wafanyakazi sita waliofutwa kazi tatizo la hali ya fedha za mishahara ziloikumba Baraza hilo lakini wafanyakazi hao hawakutaka kusikiliza kwani walighilibiwa na watu nje ya kutokana na tafauti za "kisiasa" na wakakataa kata-kata kufanya kazi na ndipo hatua ya kuwasimamisha kazi ikachukuliwa kwao.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Baraza la Lamu, Bw. Ali Mahrus wakati wa mahojiano baina yake na Mhariri wa Kiswahili wa COASTWEEK, Bw. Abdulrahman Sheriff katika afisi yake iliyoko kisiwani Lamu siku ya Jumapili iliyopita.

MHARIRI WETU, Bwana Abdulrahman Sheriff (chini) Alitembelea Kisiwa cha Lamu ambapo alipata fursa ya kuwasiliana na Mwenyekiti wa Baraza la Lamu, Diwani Ali Mahrus (juu) aliyezungumza juu ya uchafu ulioko kisiwani pamoma na kufutwa kazi kwa wafanyakazi sita.

Bw. Mahrus alisema kwamba migomo halikuwa jambo ambalo lingeliwasaidia wafanyakazi hao kutatua matatizo yao." Tulijaribu tulivyoweza kukaa nao na kuwafahamisha matatizo yanayolikabili Baraza lakini walilichukulia swala hilo "kisiasa" baada ya kuchochewa na watu nje ya Baraza hili", akaongeza Mwenyekiti huyo.

Akiendelea kuzungumzia juu ya jambo hilo. Bw. Mahrus alisema si wafanyakazi sita pekee ambao hawakulipwa mishahara bali ni pamoja na wafanyakazi kadha wa Baraza hilo. "Hivi nikwambiavyo, kuna Madiwani ambao hawajapata mishahara yao kwa kipindi cha miezi kumi iliyopita", akaeleza.

Alisema mishahara ya wakati huu kwa madiwani, wafanyakazi pamoja na makarani wa Baraza hilo imepanda kwa kiwango cha asilimia 40 ukilinganisha na mishahara iliyokuwako kwa kipindi kilichopita. "Nakubali kabisa kwamba Baraza liko katika hali mbaya ya kifedha", akasema.

Bw. Mahrus alimwambia Mhariri kwamba wiki mbili zilizopita walikutana na maafisa wa Wizara ya Serkali za Mitaa akiwemo Katibu wa Wizara hiyo na kuzungumza kwa kirefu juu ya shida kubwa inayolikabili Baraza la Lamu na akaeleza kuwa "ni jambo la furaha kwamba Lamu itakuwa mojawapo ya mabaraza yatakayopata msaada kutoka kwa Wizara".

"Shida kubwa iliyotukumba ni ukosefu wa msaada wa kifedha uliokuwa ukitolewa kwa mabaraza na Wizara lakini mara tutakapopata fedha za kutusaidia, matatizo yanayolikabili Baraza la Lamu kwa wakati huu yatamalizika na kila jambo litafanyika na huduma muhimu kutekelezwa", akasema Bw. Mahrus.

Bw. Mahrus aliye pia Mwenyekiti wa Kanu wilayani Lamu alilifahamisha COASTWEEK kwamba wale waliofutwa kazi wameshalipwa haki zao zote zikiwemo mishahara ya miezi ile ambayo hawakulipwa na pia wakalipwa mshahara wa mwezi mmoja wa notisi. Aliongeza kuwa Baraza litawaajiri wafanyakazi wengine ili waendelee na kazi ya kuusafisha mji huo wa Lamu ambao umekuwa mchafu kwa kipindi kirefu sasa.

Katika mahojiano hayo. Bw. Mahrus pia alisema alikutana na Waziri wa Utamaduni na Huduma za Jamii, Bw. Kenneth Matiba kuhusiana na tatizo la uwanja wa soka katika kisiwa hicho. "Nina furaha kukufahamisha kuwa Bw. Matiba amekubali mwaliko wa kutembelea hapa na mipango kufanyika ili tuwe na Stadium ambayo itawasaidia vijana wetu kujiendeleza kimichezo", akaongeza.

Kutokana na matatizo ya kifedha, Bw. Mahrus amesema Baraza lake limeamua kupunguza idadi ya wafanyakazi katika idara za Baraza hilo. Baraza limeamua kupunguza idadi kutoka idara nyingine kama shule za watoto (nursery). "veterinary" na katika workshop. Uamuzi umeshachukuliwa juu ya jambo hilo na Baraza linangoja kuidhinishwa wa uamuzi wake na Waziri anayehusika.

Bw. Mahrus ameiomba Wizara ya Ardhi na Makao ipatie Baraza lake umilikaji wa Ardhi. "Baraza letu halina ardhi na hii pia ni shida mojawapo tunayopata", alisema na kuwa na matumaini kuwa Baraza lake litapata misaada kutokana na Utalii.

Akimaliza mahojiano yake, Bw. Mahrus alizungumzia ubovu wa "Mabuntwa" kwa kuiomba idara ya ujenzi (MOW) irekebishe sehemu hizo na pia kutia taa kwenye mabuntwa hayo na aliahidi kwamba Baraza lake litafanya kila jitihada kuona hali ya uchafu katika kisiwa hicho unamalizika.

MHARIRI: Wakati wa ziara yangu nir iegundua hali ya kisiwa hicho bado inaendelea kuwa mbaya zaidi kwani uchafu umetapakaa sehemu kadha. Wiki ijayo nitawatolea barua nitakazopokea kutoka kwa wakazi wa Lamu pamoja na picha ambazo nilipiga kwenye barabara kadha zikionyesha hali ilivyo katika kisiwa hicho.

ILIKUWA IYE? Mabibi hawa wanatembea katika mojawapo ya "ndia" za Lamu bila ya wasiwasi wowote..... hapo awali. Lakini sasa, inawalazimu wayainue mabuibui yao kusudi waepukane na matope yaliyojaa katika "ndia" za kisiwa hicho.

PICHA: ABDULRAHMAN SHERIFF

MAZERA ATETEWA

VIONGOZI wa wafanyi kazi pamoja na wafanyi kazi wote wa Pwani kwa jumla wanamuunga mkono Bwana Alfred Mazera katibu wa Pwani wa chama cha COTU. Walimchagua wao kikamilifu na kikatiba.

Tumeshangaa sana kusoma katika gazeti moja kwamba Bw. Mazera ajiuzulu. Ajabu ni kwamba anayemtaka Bw. Mazera ajiuzulu si mwingine. bali ni Nw. Warrakah ambaye mpaka sasa anakalia kiti katika chama cha Kenya Union of Commercial Food • Allied Workers Tawi la Mombasa, kimabavu na bila kibali cha Wafanyi kazi.

SHAURI

Tungefikiria kwamba shauri ya Bw. Mazera kujiuzulu ama ya kutojiuzulu si shauri ya Bwana Warrakah kusema, bali ni offisi kuu ya COTU. Si jambo la busara kuwambia wenzako kufagia chumba chake kabla wewe hujafagia chako.

Tunamwomba Bw. Warrakah kuitisha uchaguzi Kenya Union of Commerical Food & Allied Workers tawi la Pwani Mombasa upesi iwezekanvyo ili ukweli uonekane na ili migawanyiko katika chama hicho imalizike na Wafanyi kazi watumikiwe ipasavyo.

COTU

Tunamkumbusha vile vile kwamba yeye (Warrakah) wakati alikuwa katibu wa COTU Tawi la Pwani aliheshimiwa sana kwa hivyo na yeye anafaa kumheshimu Bwana Mazera ambaye ni katibu wa sasa na ambaye alichaguliwa kikamilifu na kikatiba kwani kushambuliana Magazetini hakuwasaidii wafanyi kazi.

G. R. Maloba
MOMBASA.

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA T-SHIRT KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD No. 180.

KWENDA KULIA:

1. Samaki anuka vumba mnyama anuka........
6. Enea, kuwa kila mahali.
7. Kifaya, timia.
8. Sehemu ya kati ya chombo cha bahari.
11. Ponda, vunjavunja.
12. Herufi hizi zikitumika zamani Tanzania.
13. Ati, yaambiwa kuwa.
15. Bembeleza, rai.
17. Mwashuka, mwapu mzika.
20. Kiungo cha kukanusha.
21. Tayarisha au anzisha shamba.
22. Kiungo cha maneno.

KWENDA CHINI:

1. Nazi changa.
2. Madini itumikayo katika bunduki.
3. Aina ya mmea unaotambaa.
4. Hewa.
5. Kifaa cha uandishi.
9. Ngozi ya tunda.
10. Ni maji kisha kitu cha malazi.
14. Namna ya samaki wa bahari.
16. Aina ya ugonjwa wa pua.
18. Wakati wa asubuhi.
19. Boma kando ya nyumba.
20. South Africa.



JINA.......................................

SANDUKU LA POSTA..........................

....

Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 179

1. Miss Zulfa M. Ali, Sanduku La Posta 86259, MOMBASA.
2. Swale Hassani, Sanduku La Posta 96070, LIKONI.
3. Khadija Said, Sanduku La Posta 90130, MOMBASA.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANAno No. 179.

KWENDA KULIA

1. FARUCCI, 5. ZOA, 6. NUNUA, 7. MRAI, 8. ATAKULA, 9. UK, 10. EMBU, 12. NGE, 13. MAKAMO, 14. NI

KWENDA CHINI

1. FUNGATE, 2. UKUUKUU, 3. IZARA, 4. MARIAKANI, 7. MLANGO, 11. MJA, 12. NM

Shindano la Fumbo La kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa a mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yetakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe Feb 22 1984 Saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.